

UTABIRI WA MTHANI WA KCSE , 2024

Kenya Certificate of Secondary Education

102/2 - KISWAHILI - Karatasi Ya 2 (Lugha)

T2 2024 – MUDA 2 $\frac{1}{2}$

KCSE TRIAL
EXAMS, 2024

Jina Nambari ya mtahiniwa.....

SahihiTarehe.....

Maagizo Kwa Mtahiniwa:

- a) Andika jina lako, jina la shule yako, nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mthani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- c) Jibu maswali yote.
- d) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- e) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali
- f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
- g) Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa.
- h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	ALAMA	UPEO
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	



T2KISW2024



21123456789

FOR MARKING SCHEME CALL/WHATSAPP 0799906300

FUNGUA UKURASA

Page 1

SWALI LA KWANZA-ALAMA 15

UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:

Ni dhahiri kwamba uharamia umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vivya vivya, matendo haya ya maovu ambayo yanaweza tu kumithitishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia na nchi huska, simanzi na masaiibu yasioweza kutiwa kwenye mizani.

Yamkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azima na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mjini Nairobi na Dar es salaam mnamo Agosti 7, 1998, na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kuto sheleza matakwa yao kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala –wajibika katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za musitisha majanga makubwa kama vile njaa, umaskini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili suala linalosawisishiwa na ‘kinyume mbele’. Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazielekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaielekea kuzipiga jeki juhudi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia hausajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalani, jambo lisilopingika INpodINIK kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidhaa nuhinu zinazoendelea ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya millenia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda ya mashariki ya bara la Afrika zimejuhumiwa. Ni muhali kwa utalii kustawi kwenye

maeneo yaliyo na tishio la usalama .Itakuwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtondoo ulimwenguni ni ndoto ambayo haijaimia hata hivi sasa,kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya hindi.Kwa mujibu wa hali hii,mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni .Licha ya hayo ,shughuli za uvuvi na biashara nyenginezo kwenye kanda ya mwamba zimetiliwa shaka si haba.Itabidi mikakati na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusisitishwa.

Maswali.

- (a) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni. (alama3)

.....

.....

.....

.....

- (b) Fafanua dhana ya 'kinyume –mbele' kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 2)

.....

.....

.....

.....

- (c) Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi .Fafanua. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

- (d) Thibitisha kuwa Kenya imeathirika pakubwa kutokana na vitendo vya uharamia . (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

(e) Ukirejelea kifungu ,eleza maana ya;

(alama 3)

(i) uharamia

.....
.....

(ii) mtandao

.....
.....

(iii) mwambao

.....
.....

2. UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Ama kweli maisha ya vijana wa kisiasa yanatofautiana na kuhitilafiana pakubwa na yale ya wazee wao .Sio katika mavazi ,mienendo , mitazamo,mawazo na mieleko tu bali pia katika kipengele kingine chochote utakachofikiria.Yote haya ni vielekezo vya jinsi kizazi cha leo kinavyoishi katika ulimwengu ambao ni kivuli tu cha ule wa vizazi vilivyotangulia . Baadhi ya watu wameieleza hali hii kuwa maisha sio jiwe .Kwao basi ,si ajabu katu kuwaona vijana vijana wakizungumza lugha yao ya kipekee au wakivaa nguo zinazobana ajabu na kudhihirisha bayana maungo yao badala ya kuyasitiri.

Hata hivyo ,watu wengi wameonelea kwamba hali ya maisha ya vijana wa leo ni maasia yanayotokana na utundu na hata ukatili wao.Upande huu umetoa rai kwamba kizazi hiki kisingepotoka kama tu kingezingatia na kustahi utamaduni wa wahenga wao ambamo wazazi wao ndimo walimokulia.Wanazidi kufafanua kuwa nyendo hizi za miaka ya nyuma zilithamini sana amali kama uaminifu,heshima kwa wazee ama wakuu,bidii,ushirikiano,ukarimu,unyenyekevu,hadhari katika kila jambo ,utilifu na pia kujitegemea .Yote haya yamesahaulika ama tuseme yamepuuswa katika “utamaduni wa kisasa”.

Swali linalokuza sasa ni je,tunapaswa kuwahukumu vijana wa leo kwa kutumia vigezo au masharti gani?Tuwapige darubini kwa kutegemea hali ilivyo hivi leo duniani ama tuwapime kwa mujibu wa jinsi maisha ya baba na babu zao yalivyokuwa.Jibu la swali hili ni gumu na sharti lifafanuliwe kwa makini lisije likaegemea upande wowote.

Mathalani ,ni jambo lisilopingika kuwa maisha ni utaratibu unaoathirika na hivyo kubadilika daima.Angalia kwa mfano jinsi maendeleo ya elimu ,sayansi,mawasiliano na hata ufundi yalivyoyageuza maisha siku hizi.Yamkini vijana wa barani Afrika wakaona na hata kuzungumza kwa wenzao kutoka Uropa,Asia na Marekani bila hata kunyanyuka hapa kwao nyumbani .Athari ya filamu,video ,vitabu ,magazeti ,majarida na kadhalika haikadiriki.Haya ,kwa kiasi yamewafanya vijana hata kupevuka kabla wakati wao.Isitoshe, mambo haya yameweza kuwazuzua na kuwaaminisha ya kuwa yale wanayojifunza ni kweli.Matokeo yamekuwa ni wao kuudunisha utamaduni wao wa asili na kuupapia ule wa wageni waliowaathiri .Tusisahau kuwa ujana ni tembo la mnazi na rahisi kwao kubadili mawazo.

Lakini hatuwezi kuwasamehe vijana wanaokosa akili razini kwa kupotoshwa na kucharika na yote wanayoyapokea kutoka ugenini na hivyo kuanza kudhalilisha utamaduni wawaafrika.Hata hivyo ,badala ya kuwakashifu wanapopotea njia ama kuwapongewa wanapotenda yale tunayoyategemea tu,ni wajibu mkubwa wa wazazi kuwaongoza na uwezo na kufanya utezi mwafaka katika maisha yao.

Maswali.

- (a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa kifungu ,fanya muhtasari wa aya ya kwanza na ya pili.(Maneno 40) (alama 7)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

- (b) Fupisha aya mbili za mwisho .(Maneno 50) (alama 8)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vielezi viwili vya silabi moja. (alama2)

.....

.....

b) Onyesha sifa bainifu za sauti zifuatazo (alama2)

i) f/v

.....

.....

c) Ainisha mofimu:Awaibiaye (alama2)

.....

.....

.....

d) Eleza huku ukitoa mifano matumizi mawili ya kiambishi ‘ji’ (alama2)

.....

.....

.....

e) Huku ukionyesha upatanisho wa kisarufi weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka (alama2)

i) Uwele

.....

.....

ii) vita

.....

.....

f) Tumia ‘o’ rejeshi tamati kuunganisha sentensi zifuatazo (alama2)

(i) Jino linauma

(ii) Jino limeng’olewa

.....

.....

g) Tambua vivumishi na uonyesha ni vya aina gani .

Wanafunzi wawa hawa waliochelewa watafanya kazi ya sulubu kama adhabu. (alama3)

.....

.....

.....

.....

h) Kanusha: Msichana ambaye amefika ametuzwa (alama 1)

.....

.....

i) Onyesha aina za virai katika sentensi hii:

Wale wazazi wetu watawasili kesho saa tatu (alama2)

.....

.....

.....

j) Unda nomino kutokana na kitenzi ‘Haribu’ (alama1)

.....

.....

k) Tambua aina za vitenzi katika sentesi,

Hawa sio wachezaji waliokuwa wakicheza jana (alama3)

.....

.....

.....

l) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya viunganishi vya kulinganua (alama1)

.....

.....

.....

m) Eleza matumizi mawili ya 'ka'Toa mifano katika senstensi (alama2)

.....

.....

.....

n) Andika visawe vya maneno yafuatayo (alama1)

i) Daawa.....

ii)Ainisha.....

o) Jaza nafasi zilizoachwa (alama2)

_____	liwa	liana
Hoji	_____	_____

p) Andika kinyume: Tajiri aliyesifiwa amelaaniwa (alama1)

.....

q) Changanua sentensi hii kwa kutumia vishale

Yule mgeni aliyefika jana ameondoka leo (alama3)

.....

.....

.....

R) Tambua vishazi na uonyeshe ni vya aina gani

Rudisha atapendwa na wengi ikiwa atashinda leo (alama2)

(alama2)

Sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadillika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote alivyorukia. (alama3)

.....

.....

Eleza makosa matano yanayoweza kutokea wakati wa mazungumzo . (alama10)